

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report Of

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, NORTH MUGIRANGO
BORABU CONSTITUENCY, EKERENYO DIVISIONAL HALL**

ON

9TH OCTOBER 2002

Transcribed by Lillian Momanyi

Final Draft

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, NORTH MUGIRANGO BORABU CONSTITUENCY
HELD AT EKERONYO DIVISIONAL HALL HELD ON WEDNESDAY 9TH OCTOBER 2002**

Present

1. Com. Pastor Zablon Ayonga

Secretariat Staff in Attendance

1. Lydia Manyoni – Asst. Programme Officer
2. Vivian Muli – Verbatim Recorder
3. James Masaki Mong'are – District Co-ordinator

Meeting was called to order at 10:30 a.m.

Com. Ayonga: *Ninki mokomiganera igabu ne ebirogo biichere iga? Igo ntagete abanto bosu bwane iga. Ninki mokomiganera igabu? Ikaransa gochiaa. Nabaria more nyumba inchu iga kamoranche. Ninki gaki mwanchera kobera ari iga mwatetenti abantu chibenchu chiichire iga? Ninchwo iga.*

James Masaki Mong'are: *Ikaransa gochia, kei! Abagochaa tigabana goikaransa gochia magegega.*

Com. Ayonga: *Eeh bono.*

James Masaki Mong'are: *Abanto ba minto bwakire mbuya more?*

Response from the audience: *Eeh bwakire, mbuya tore.*

James Masaki Mong'are: Yes, I think we can now start our meeting and I want to request that we all stand and have a word of prayer from Mzee Charana.

Mzee Charana: *(Prayers) Nyasae oito, mbuya mono aseng'encho yo obuya bwago na mbuya mono ase enng'encho yo obomoyo gwatoretire mpaka rituko ria rero. Kwa rorire abarai baito be Constitution bachire ase rituko ria rero ase engencho yo gototebi na ninki keru kendererete asengecho ye katiba. Nyasae oito twasabire chingati echi iga ekero twachakire omokutano oyo, obe omonyakerogo, tochake buya, naende tokore buya. Onsi otwa sabire na twaegenire gwatoigire ekiagera twasabire goetera ase obuya bwa Kristo oyo re omochenu, Amen.*

James Masaki Mong'are: Thank you very much. Let me take this opportunity to welcome each one of you to this meeting. It is a meeting that I must admit as the Co-ordinator that we organized rather haphazardly but more important than that I think I am extremely happy that even within that short notice, that you have been able to respond in the manner in which you have done.

With that therefore, allow me, I know you all know the purpose of the meeting. You read that on paper, it was on radio, we have even gone round this morning and yesterday telling people about the function. But when time for the Commissioner comes I am sure he should tell us why we had to have this function.

Before the Commissioner comes to talk to us, I would like you to allow me to introduce my office assistant, Helen Nyakoni. This is a lady who we have worked with in Nyamira and I am sure you know my name, my name is James Mong'are, I am the District Co-ordinator, co-ordinating this exercise of reviewing the Constitution.

Before us here we are happy to have with us Commissioner, Pastor Zablon Ayonga, who has come on behalf of the Commission to oversee this exercise. So Commissioner, karibu, karibu sana.

Com. Ayonga: Thank you.

James Masaki Mong'are: Just as I seat down, Bwana Commissioner, this is North Mugirango, Borabu Constituency and I must report with a lot of pride that during the period of views gathering, this Constituency was extremely active. Very, very active and this is one area where we collected very focused views which have now found their way into the Constitution that is in the process of review. So, this is the Constituency that has been extremely responsive in this exercise of reviewing the

Kenyan Constitution. We have not had any problems and I am sure you can even feel a change from the faces of the people we have before us.

So, allow me therefore with those few remarks to welcome Pastor to introduce to us the members of staff with whom he has come down here with from Nairobi. And then to tell us why the function of today had to be organised. Commissioner.

Com. Ayonga: *Bwakire mbuya more mwensi?*

Response from the audience: *Mbuya mono.*

Com. Ayonga: I want to take this opportunity to introduce to you the staff I have come down with from the Secretariat. I have Ms Lydia, she is our Programme Officer, she is a lawyer and she is going to assist me. *Lydia kwania abanto ba minto.* She comes from Keumbu, Nyaribari Chache and she is working with us in the exercise. Then with her is Muli Vivian, she has come from the Secretariat, she is the Verbatim Recorder and she is going to record any views that you might have. Then we have two other ladies, stand up and introduce yourselves. They have to observe and see what goes on.

Number one, I have been here before. I have been here at the school and this morning I had hoped I was going back to the same place only to be told right here by my driver that he was told yesterday that the place was burnt down and that there is no (inaudible). And I am sorry for what must have happened there, but then work must go on.

I remember that particular day and that day, that ka-hall there, was full to the capacity. Where are those people? Those people who gave me their views? Because, today's meeting is to reflect and focus on the views that you gave us that is the reason why we have come down here. And I noticed you have taken the Katiba, which is a draft. In order to consult that, I would like for you to listen to me without being busy reading. Actually you should have gotten this material earlier so that you read it and then when I come, like I have come then we would talk.

But unfortunately, things didn't work they way they have worked. Of course now you have it, *more na amaiga yo korora ime nga ninki bono eke kegakare iga?* At the same time I am talking to you. You will have divided attention. Before I start how many of you do understand English? Thank you. How many of you do not understand or cannot follow the conversation in English? *Oyomo bweka? Two? Monu ki motagete nkwane?*

Is there anyone who does not follow *Ekegusii*? Because I want to cater for everybody. I just want to be sure that the kind of crowd I have what kind of language am I going to use? Okay, I will use a mixture of everything. *Egento nareng e gosaba*, for those of you who have got the Draft Katiba, if you could set it aside for a while so that after I have talked you can look at it, *tekoba buya?*

When I came here last time, at that Girls Secondary School, we gave you a chance to talk, to tell us what you want and you told us what you wanted. Then we told you, that we have recorded your wishes, what you would like a Katiba be like. And that we would go back to Nairobi, after we have collected the views of everybody, then put these views together. Many views have been similar, what you thought was your problem was the problem of a Kipsigis, of a Kuria, of a Luo, of everybody in Kenya. And so all those views have been reflected in that report, which you should have read but unfortunately you haven't.

Now, I want to take you through some of those important features that you might see, which we have put down in writing to make a Draft Constitution. What you have there is not the real thing. You see we call it a 'Draft', why do we call it a 'Draft', because you haven't looked at it, because the National Conference has not met to say this is what we want and then it becomes a Katiba.

Bono ne egentu mogosoma erinde morigereri eeh, eke nkeri twatebete. Eeh, omochando oyo noro oria twabwate. Ndio, oyo mbuya orikire, lakini iga haukuandikwa sawa, sawa. Hapa sielewi. Mnaanza sasa ku-debate au jambo fulani, fulani lililokuwa na maana sana halikuandikwa, limesahaulika. Nimeanza kuona Atwoli, huyu COTU Secretary General anaanza kusema kwamba maoni ya wafanyikazi hayakupewa uzito. Hamjasoma hiyo, simumesikia hata katika redio? Yeye amesema hayakupwe uzito, na sisi tunasema yalipewa uzito unaofaa.

Lakini kwa maana sasa ni wakati wa kuangalia kilicho andikwa na ambacho hakikuandikwa, nut ambayo haikukazwa sawa sawa au ambayo imekazwa zaidi. Kama ambavyo majudge wanasema ooh, hawa watu wameanza kutukata miaka, hawa watu wameanza kutuita majina, hawa watu wanataka hivi na vile na hii hatutaki. Hiyo ni Sheria. Lakini vitu ambavyo tumeandika ni vile tulitoa wapi, kwenu.

Maneno ya majaji ambayo tumeandika ni yale ambayo tumekusanya kutoka kwa wananchi. Wananchi wanasema hivi, wananchi wanasema hivi. Wananchi wanasema kuna corruption, na kama kuna corruption ni sisi tutaandika jina lingine? Situtaiita tu corruption? Basi ni juu yako kama unaona hiyo haikuwekwa ufike kwa National Conference na useme hapana hapo mlivyosema hivi, hii haikuwa namna hivi, hii ilikuwa namna hii. Lakini sisi tumeandika maoni ya wananchi ambayo wametupa.

Nikianza ili nifuate orodha ambayo ni ya Constitution hii, Draft ambayo tumefanya. Mlisema kwamba katika ile Constitution ya zamani hakuna preamble. Hapa kwenu mlitaja neno hilo la preamble? Lilisemwa? Na tukaenda pahali pote katika Kenya nzima na kila pahali tuliambiwa hamna preamble, hamna preamble katika hii Constitution ya sasa.

Na sisi tukaenda ndipo tukasema wananchi wamesema tuweke preamble. Na sasa mimi ninawasomea yangu hapo na hamtakuja kuona hapo. Ndipo tukaenda tu, tulipoangalia samples which people gave us, we came to draw one preamble na

tukasema “We the people of Kenya, aware of our ethnic, cultural and religious diversity, and determined to live in peace and unity as one indivisible sovereign nation. Committed to nurturing and protecting the well being of the individual, the family and the community within our nation. Recognizing the aspirations of our women and men, for a government based on the essential values of freedom, democracy, social justice and the rule of law. Exercising our sovereign and inalienable right to determine the form of governance of our country and having fully participated in the Constitution making process, to our draft. Enact and give to ourselves and to our future generation this Constitution. God Bless Kenya. We came to that.

There were so many samples because you asked us, give us a preamble, which focuses, to our State and then we came out with that in this Draft. So we fulfilled one thing that you wanted. You may not have wanted it like that but after reading several samples of preambles, we have come out with this.

Now, next to the preamble, you told us to state clearly who is sovereign and we said, the people of Kenya are sovereign. The sovereignty of this country belongs to the people. and you told us, that the Constitution is supreme. Hakuna mkubwa kwa Constitution, watu wote katika Constitution ni nini?

Response from the audience: Ni sawa.

Com. Ayonga: Mkasema ni sawa. Kwa hivyo sote tutawaliwe na nini? Na Katiba. Nasi tukasema kuna chapter one ambayo inaongea juu ya sovereignty of the people, supremacy of the Constitution, enforcement of the Constitution, defence of the Constitution and the laws of Kenya. Hivi vitu vyote put together vinawafanya watu wote kujijua kuwa sisi sote ni Wakenya na tuko chini ya Katiba. Hakuna mkubwa, hakuna mdogo. Hakuna maskini, hakuna tajiri. Watu wote under the Constitution are what, they are equal.

Ndipo chapter 2, tunaongea juu ya declaration of the Republic, territory ya Kenya iko mpaka wapi, capital ya Kenya ni nini, you may ask. Watu wengine walituaambia, pengine hapa kwenu hamsemi. Mnajua kwamba capital ya pahali inaweza kubadilika wakati wowote? Mnajua nchi zingine capital yao inaweza kubadilika kwa maana haikuwekwa kwa Constitution? Na sisi tukaweka lazima capital ya nchi yetu iwe katika Constitution ili kesho fulani asije aseme hivi, ‘sasa mimi Nairobi sio inaweza kuwa capital, mimi ninataka kuleta capital Nakuru, au ninataka kupeleka capital Kisumu, au ninaweza kupeleka capital Eldoret,’ pahali popote, hata Garissa, whatever.

Na kwa hivyo tukaipanda katika Constitution. The capital of this country ni wapi, Nairobi. Kwa hivyo hakuna mtu ambaye anaweza kuitoa. Akiitoa atakuwa amevunja nini, Sheria na Katiba ya nchi. Mnaona jinsi Nigeria, si walihama wakaenda huko kwingine, wakaenda Abuja? Zamani tulijua wapi? Lagos. Sisi tumesoma shule tukijua capital ya Nigeria ni Lagos. Haya maneno mengine haya sisi hatukujua, lakini ilihamishwa. Tanzania tulijua capital ilikuwa wapi? Lakini sasa ni wapi? Unaona umesema Dodoma tena ukasema Arusha. Unaona, vitu ambavyo vinaenda namna hivyo, ni kwa maana Constitution

haikupanda hicho kitu kiwe kigumu ijulikane kwamba ni hivyo. Kwa hivyo tuliweka katika Katiba capital yetu ni Nairobi.

Halafu language, unajua kwamba language pia inakuwa shida? Mlituambia kwamba language lazima tuwe na two official languages; Kiingereza na Kiswahili. Na national language iwe nini, Kiswahili. Na tukajua kwamba jambo hilo lazima liwekwe katika Constitution. Lisiwe jambo tu la kusema lakini liwekwe, ili kesho mwingine asije asema hapana na lugha hii lazima mjue.

Kwa maana unajua mtu akitawala an akiwa na uzito wa nguvu, mnaweza kuambiwa lugha nyingine. Kwa hivyo vitu kama hivyo tumeweka.

Halafu, mlituambia juu ya the State and religion. Kuna shida katika nchi zingine za ulimwengu ambako dini inakuwa dini ya taifa.

Mmejua nchi kama hizo? Kama ipi mfano? Mnaona watu wengine, Sudan mnaona uko pande za juu ni Waislamu na chini? Na kuna nini?

Response from the audience: War.

Com. Ayonga: War. Nigeria tunasikia sehemu zingine ni nini, Kiislamu na zingine ni Wakristo. Kwa hivyo kuna vita, kuna vita kwa maana nchi zingine zimefanya religious State. Na sisi tukasema hapana, jinsi mlivyotuambia. Tukasema watu wetu wanasema State ni State na dini ni dini. Kila watu waabudu jinsi wanavyoweza kuabudu. Kwa hivyo msije mkaleta mambo ya Serikali na mkachanganyana ndio Serikali inatawala na inatawala dini. Kwa hivyo si hayo mambo tumeyaweka na mlituambia, ama nyinyi wa hapa hamkutuambia?

Halafu kuna mambo mengi ambayo tumeweka hata siku za kupumzika. Ni siku gani ambazo ungeita national days, ni siku gani ambazo zingekuwa hivi na hivi. Kwa hivyo mtakuja kuona mtakapo soma, mtakuja kuona suggested days ambazo zimeitwa national days. Kwa maana tusije tukaacha a loophole, fulani kesho akija naye afanye siku yake, mwigine akija siku ingine naye afanye siku yake. Hiyo itakuja kuwa na national days nyingi na zingine zianze ku-lose meaning.

Ndipo mlituambia tena juu ya citizenship. Wengi mlituambia juu ya watoto kuoja nje, kijana wako ameenda ameoja uko America, ameenda huko India akaoa, ameenda sijui wapi akaoa. Akaja na bibi na bibi ana shida, sasa huyu bibi anaitwa nini? Na sisi tungependa akiletwa huyu bibi naye aitwe Mkenya, si mlituambia mambo kama hayo? Mtakuja kuona hayo yamemulikwa katika masomo ambayo mnayosoma. Tumetaka hawa watu wote wawe na haki.

Mkatuambia juu ya haki za citizenship za watoto. Mtoto huyu amezaliwa na watu rangi mbili, sasa huyu mtoto naye atafanywaje? Kuna watoto ambao wamezaliwa hapa Kenya na hakuna wazazi nyinyi. Je wangepanwaje wakati tunapofanya kazi ya uraia? Kwa hivyo mambo hayo yote yamemulikwa katika Katiba.

Mengine ambayo mmetuambia ni juu ya Bill of Rights, Haki za Mtu bila ya kubagua mtu mwingine. Wakisii au wanaume mara

nyingi wanabagua wanawake. Si mmesikia wanawake wakilia kwamba wamebaguliwa?

Response from the audience: They are not here.

Com. Ayonga: They are not here. Ni kwa nini pengine hawako hapa? Hawako hapa, na hao pia unaona mara nyingine wanajibagua kwa maana wanajua wanabaguliwa, wamezoea kubaguliwa.

Speaker (from the audience): Hata hapa ni wanaume tu.

Com. Ayonga: Hata hapa ni wanaume tu. La kuna mama huyo, huyo mama yuko hawa kina mama wako. Unajua hata lugha yetu hii ya Kikisii unasikia mtu anasema kama ulikuwa unaenda pahali na unauliza umekutana na watu kwenda hapo? When they mean watu they mean who?

Response from the audience: Men.

Com. Ayonga: Men. Wanaweza kukuambia, la sijakutana na watu kwenda upande huu nimepata tu wanawake. Au nimepata mtu mmoja na wanawake. You see ubaguzi wa namna huo ambao umeingia hata katika lugha yetu ya kuongea ya kawaida. Tumeanza kuweka kwamba kila mtu ana right ya kuishi, right to life.

Kila mtu ana haki. Mzee, kila mtu ana haki ya kuishi, ya kuwa hai. Kila mtu anahaki ya kulindwa. Kila mtu anahaki ya kupata mali, kuzalisha mali na mali kuitwa yake. Tunaubaguzi ambao hata sisi wazazi tunawapa watoto wetu. Mtoto msichana, Wakisii hapa tunapogawa mashamba tunagawia nani?

Response from the audience: Wavulana.

Com. Ayonga: Lakini mlituambia, kama nyinyi hapa hamkuniambia nilipokuja hapa lakini niliambiwa pahali pote ambapo tumezunguka Kenya. Kenya nzima inasema kila mtoto agawiwe mali ya baba yake. Kama wewe bado ungali unafikiri kwamba mtoto asigawiwe mali, umechelewa, umechelewa. Watoto wote ni wako. Kwa hivyo mzazi anapogawa mali yake ama mali yako lazima kila mtoto aridhi. Unajua kuna zile siku mzee, siku zile zenu zamani kidogo, kila msichana alikuwa anaolewa. Siku hizi kila msichana anaolewa?

Response from the audience: Hawaolewi.

Com. Ayonga: Na atakwenda wapi? That is the question. Mimi nilifikiri ni hapa Kisii tu tumeanza kuona wengi hawaolewi, lakini nikapata kote ambako nilikwenda. Wasichana wako na hawakuolewa. The question is what do you do? Tukasema

katika Katiba, kila mtoto anahaki ya kuridhi mali ya baba yake. Lakini tena ujue hivi, nimepata kwamba watoto wasichana ni wazuri sana, ni wazuri sana. Kwa maana pahali pengine tulikuwa tunaambiwa hivi, ninadhani hapa Kisii, sitaki kuambiwa pahali niliambiwa habari hiyo na nikafikiria iko important.

Ambako pahali tuliambiwa, na ilisemwa na Mkisii, *agoteba nga, abagaka tiga baagacherwe omochie bwa abagaka na abang'ina. Ikiagera abanto aba babeire enuisance. Mwaigure egento ekio? Moigwete egento ekio? Ng'a abagaka ekeru kwagotire, karubwogo, urusigwe bwogo, uchie obekwe omochie, obweri bwa abagaka abanto baria abagotu. Obere oo goika orue ense eye. Timbabwati ribaga ria ogokorenda, abu bagoteba mbanto ki? Abana bago. Tibabwati ribaga, they are busy working, eeh. Na ogokorenda is very expensive! Mbuya obekwe ase ebomeyuo oberee oo chinsemo chinde, ee bono nao ogochia kokuera.*

Chinsemo chinde tobwate, nyumba za wazee. Si zinaitwa hivyo? Nyumba za wazee. Kwa hivyo tunasema kila mtu ana haki ya kuishi. Na hata tukaweka, kuna section inayodeal na hawa senior citizens, wazee wetu. Awe na mali yake, afanye apendavyo na mali yake na ikiwa anauwezo wa kuchangia Taifa, na achangie. Kusiwemo discrimination. Tumeanza kuiga tabia tu za watu wengine huko, za kizungu ambazo ni mbovu. Watoto hawabarikiwi na mababa zao, sasa mzee unabebwa kutoka mji wako kwamba kwenda huko, kwenda huko, na unafungiwa uko ni kama mtu yuko korokoroni. Utoke boma yako uende huko korokoroni ukae huko.

Kwa hivyo tuna rights hizo na kuna right ya kuwa sawa na watu wengine. Na haki ya wanawake kufikiriwa kama watu, sio mwanamke tu bali kama tu ambaye anaweza kuchangia Taifa. Mwanamke anaweza kuwa na mali yake, yeye mwenyewe na yakaitwa yake, na akafanya apendavyo na mali yake ikiwa atafuata Sheria. Kuna haki ya kuoja, kuna haki ya kuolewa, kuna haki ya kuishi jinsi unavyo taka, bora usivunje Sheria.

Kuna haki ya walemavu. Mtu hakulemaa kwa kupenda kwake, amelemaa kwa jinsi ambavyo yeye mwenyewe hakuchagua kulemaa. Mwingine amekuwa mgonjwa akalemaa, mwingine amepata ajali akalemaa, na mwingine amezaliwa akiwa mlemavu. Lakini mtu katika hali yoyote anahaki ya kuhudumiwa kama mlemavu, ya kupewa kazi kama mlemavu, ya kuishi kama binadamu mwingine katika vile vitu ambavyo anaweza na kufanya kazi kwa mambo yale anaweza. Hayo yote tumeyaweka.

Heshima ya mtu, kwamba mtu ni mtu, mtu sio mnyama. Kama hii sasa unianza kuana watu wanabeba watu juu ya carrier ya matatu. Unaona zile carrier ziliwekwa huko juu ya matatu, ziliwekwa za nini?

Response from the audience: Za kubeba mizigo.

Com. Ayonga: Na siku hizi unaona nini?

Response from the audience: Zimebeba watu.

Com. Ayonga: Unaona binadamu. Lakini binadamu amechagua kufanya yale mambo. Binadamu amechagua kufanya hayo mambo, mambo ambayo sio sawa. Ile sio dignity ya binadamu, binadamu anawekwa huko kwa carrier. Hata huduma ambayo inayopewa wanyama haifanywi namna hiyo. Kwa hivyo hapa tumeweka, kuna human dignity. Haki ya binadamu kuwa na security, freedom of security, kila mtu anahaki. Hayo yote yamefall under the Bill of Rights.

Kuna habari ya privacy, mtu aishi hiti tu kama mtu yuko uchi, lazima mtu anaprivacy yake. Unahaki, unahaki ya kuwa na privacy. Freedom of religion, and of opinion. Mlituambia kwamba Uhuru wa kuabudu, na huu umesemwa kwa kila constituency ambazo tulikwenda. Haki ya kuabudu. Na sasa tumeiweka katika hii Katiba. Utakuja kupata kwamba tumesema hakuna mtu yeyote atakuwa compelled kufanya kazi wakati ambao inampasa aende kuabudu. Na hii mlituambia juu ya watoto wa shule ambao wakienda shule fulani, fulani wanaambiwa leo ni kazi, wengine mnaenda mnasema mnaenda Sabato, hakuna hicho kitu mnatuambia Sabato. Kama ulikuwa unataka Sabato hiyo, kwenda hiyo shule yenu inayo fanya mambo ya Sabato.

Au siku ya Jumapili, huyu mtoto analazimishwa kwenda kufanya kazi. Au mfanyikazi, wengi wamefutwa kazi zao kwa maana hafanyi siku ya Sabato. Kuna zile benki ambazo zinafanya siku ya Saturday moja sijui in a month, na kama ulikuwa unafanya huko na kama pengine wewe ulikuwa cashier au whatever au teller, unaambiwa kwamba kama hauwezi kufanya kazi siku hiyo, mambo yako yatakuwa namna gani? Yamekwisha.

Na tunasema katika hii Katiba mpya, hakuna mtu ambaye atakuwa compelled kufanya kazi. Hakuna mtu ambaye atanyimwa employment kwa maana ya dini yake. Watu wengi wanapiga lami kwa maana akaitwa kazi akaona kazi imetangazwa huko, akienda kutafuta hiyo kazi, well qualified to take that job, lakini unaambiwa utafanya siku hii au the first week of that which you got, unaenda ukamwambia boss wako kwamba, kesho unajua boss, sitakuweko kazini. Boss anasema kama hutakuweko kazini, you are through with us. Si hayo mambo yamefanywa na mlituambia, na tumeweka katika Katiba.

Freedom of opinion, freedom of expression, access to information, assembly, demonstration na political right. Ukichagua unataka kuwa na chama chako, unahaki, bora tu umepata following ya kutosha. Freedom of trade, occupation and profession. Unaright ya kuwa na property, ku-own property. Unahaki ya kupata matibabu. Mara nyingi mlituambia kwamba siku hizi hata ukienda hospitali hakuna dawa. Unaandikiwa tu kakaratasi hivi na unaambiwa enda pale ile chemist uko chini na hiyo chemist ni ya mtu huyo huyo, ndipo unaenda kununua dawa. Hayo yote tumeweka katika Katiba, mambo ambayo utakayo soma. Freedom to education, housing, chakula, maji, usafi na hali ya mazingara. Vyote hivyo viko katika chapter 5.

Na katika chapter 5 kuna mambo mengi, consumer right, right not to obey unlawful instruction, hata hiyo tumeongeza. Kama mambo unayoambiwa sio mambo mazuri, you don't have to obey, utakataa kama hayalingani na Sheria. Ile habari ya kugandamizwa, mtu anachukua kuku yako, anashika kuku, tu hiyo kuku inakibishwa inakwenda huko kwamba ilete hapa mimi

niende kumchinjia fulani, tumekataa kwamba hiyo kuku haiendi, tumekataa. Unlawful instructions.

Tumeingilia hata haki ya fair trial. Mtu anashikwa tu na anawekwa kambi tu, hapo ndipo anapokaa na hajafikishwa kortini. Mlituambia kwamba hiyo inawasumbua. Mtu unashikwa tu unawekwa hapo, unawekwa tu na hakuna anayejua, na ni lazima uambiwe umeshikwa kwa nini. You must always be told umeshikwa kwa hii, kulingana na Sheria. Na pia ufikishwe kortini, sio habari ya kuwekwa kando kando hivyo. Hayo mambo yenu yote tuliweka. Kwa maana ndiyo tunaita rights of persons held in custody, hiyo mliyotuambia. Tena unahaki ya kuongea na wale Human Rights Commission na kuwaambia wakati ambako rights zako zimekuwa interfered with.

Pia mlituambia habari juu ya elections. Tumeandika yote juu ya elections. Mkatuambia mnataka voting inapofanywa papo hapo, votes zihesabiwe papo hapo. Basi tukaenda tukaweka jinsi mliyotaka. Papo hapo zihesabiwe, na watu wote wawekek sahihi kwamba fulani atapata hizi, huyu akapata hizi, huyu akapata hizi na maneno yenu yanaishia hapo. Sio habari ya kubeba sanduku kutoka hapa Ekerenyo ikimbizwe huko, ikaenda iko na ikija kufika Nyamira imekuwa kitu kingine. Sasa situlifanya kazi yetu?

Response from the audience: Ndio.

Com. Ayonga: Temefanya? Na kama iko pahali ambako utakuja kusoma hiyo pole pole na ukaona iko pahali ambapo hiyo useme sio sawa, kuna ule mkutano ambao unaitwa National Conference. Mmeshasikia kuhusu huo mkutano?

Response from the audience: (inaudible).

Com. Ayonga: Mmeshasikia juu ya huo mkutano? Mmesikia. Mnajua jinsi ambavyo niliwaambia wakati ule. Sisi baada ya kuyakusana mambo yenu ambayo mliotupa, tutaenda tuketi tuandika haya maneno, tumeandika. Halafu baada ya kuandika, tunawapa haya mambo tumeandika myasome, myasome kwa siku ngapi? Thelathini! Kuna mwezi mzima wa kuyasoma hya mambo.

Halafu tarehe ishirini na saba ya mwezi huu, ikiwa mambo hayatageuka, ninasema ikiwa kwa maana hapa Kenya yetu mambo yanakwenda namna hiyo, huwezi kujua. Lakini tunaomba na kuamini, kumwomba Mungu kwamb atusaidie mambo yaende jinsi yanavyo takikana kuenda. Tafadhali, umejiandikisha kule nje mzee?

Speaker: Eeh.

Com. Ayonga: Asante. Tunaomba kwamba baada yetu sisi kuandika haya, Wanakenya wote wamepewa siku ngapi, thelathini. Za kusoma na za kushauriana nyinyi wenyewe. Halafu mkaanza kusema sehemu fulani hii hatuitaki, au sehemu fulani hii ni ngumu sana, hii itatumiza kama ikiwa namna hii. Ingawa watu engine waliona namna hiyo, lakini sisi tunaona hii

itatumiza. Ndipo tutakuwa na mkutano, ule wa watu mia sita, sijui iko makumi mangapi.

Huo mkutano utakuwa represented na two hundred and ten Members of Parliament. Watakuwa in attendance to this meeting, 210. Halafu kutakuwapo three district representatives, ambao watakuja katika huo mkutano. Halafu tutakuwa na viongozi wa makanisa ambao wamechguliwa, ambao watakuja pia katika huo mkutano. Together watakuwa mia sita na kitu, na watu hawa watakutana for a month. Kutafuna maneno haya word for word, mstari kwa mstari, page by page, na kumaliza haya mambo.

Wakikubaliana, basi, mambo yataenda parliament. Lakini wasipokubaliana katika mambo fulani, fulani, mengine watakubaliana na kutambia sisi tuliitengeneza hii kusema hii section fulani, fulani, this we want it out. Hii haiwezi kufanya kazi, toa hii na hii, au hapa mliyoweka ni machache, tunataka include this and that. Na tutaenda tufanye hivyo. Lakini ikiwa watakataa hao wenyewe kwa kupingana kwao, sisi sasa huko tutakaa tu, hatusemi kitu. Sisi tutaangalia na macho, kusikia na masikio jinsi ambavyo wanadebate juu ya hii.

Ikiwa kutakuweko na mambo magumu ambayo hawa representative watakuja kataana kabis na kusema I don't like thins na huyu mwingine anasema this is what I want, na mwingine anasema this is what I don't want. Basi itakuwa ni nani ataamuwa watu wakiwa namna hiyo? Mnajua ni nani atakaye amua? Ni nyinyi. Mnakumbika hapo kwanza niliwaambia ni nani sovereign hapa Kenya?

Response from the audience: Mkenya.

Ni Wakenya. Na ikiwa representatives wamekuja kule na wakashindana wakawa hawakukubaliana juu ya jambo fulani muhimu, basi tunasema throw it back to the people. The people out there are very important, let them go, vote about this. Na sasa hiyo tunaita referendum. Tunatumaini haitakuwa necessary kufanya referendum. Kama kutakuweko correction, tunatumaini zitakuwa zile corrections pengine za maneno au pengine za kutoa kipengele fulani na kusema it is not necessary. Au hii, it is good lakini hii inatuacha kwa wakati huu. Lakini kama hawatakubaliana basi back to the people.

Lakini wakikubaliana, sisi tutaenda tusafishe hiyo kwa kalamu pahali ambako wamesema hii itolewe, hii iongezwe, twende tufanye hiyo. Na ikiwa tayari tunampa Attorney General apelize sasa Katiba hiyo, draft hiyo kwenda kwa parliament. Parliament ambao ni hao watu mia mbili na kumi ambao juzi wamekuwa nayo haitakuwa ngumu sasa ikienda kule kwa maana it is the same, same thing ambacho watakuwa wamekuwa wakifanya that past one month. Kwa hivyo itapitishwa.

Hao wakiipitisha, basi itaenda kwa Rais kufanya nini? Kuweka kidole. Akiweka kidole sasa hiyo inakuwa Sheria ya Kenya ambayo itawalazimisha Wakenya wote kuifuata. Na tunaoma Mungu kwamba ifanyikane hivyo. Kwa sasa mnaona kuna vita vya maneno, vita vya kusema wengine wanataka elections zije haraka na zifanyike chini ya Katiba tuliyonayo. Na wengine wanasema la, tungoje hii Katiba mpya ilitutumie katika elections. Ndio maana yake ninasema tumwombe Mungu atusaidie,

kwamba njia ipatikane ambayo Katiba hii inaweza kuingia.

Kwa maana hii jinsi mlivyotuambia, mlisema kwamba, kwanza mnaona tumeiita jina. Mnaona 'Choice of the People'. Ni uchaguzi wako, maneno yaliyomo hapa ni yako. Na kwa hivyo maneno yako haya tunataka uyafanyie kazi.

Tumesema kuwe na President, mlituambia hivyo. Mlisema kuwe na President aliyechaguliwa na watu. Na pia kuwa na Vice President, aliyefanywa nini, aliyechaguliwa na watu pia. Kwa nini, tukawauliza ni kwa nini mnataka hivyo? Mkasema kwamba Vice President hana kazi, yeye anaweza kufutwa akaachwa njiani. Lakini tunataka Vice President ambaye ni sisi tuliyemchagua. Na yeye anaweza kuendelea na term yake of service mpaka miaka mitano ile ikaisha. Kwa hivyo tumefanya hivi.

Mkatuambia mnataka, kuwe na Prime Minister na tukasema ndio. Katika Katiba hii kuna Prime Minister na kuna deputies wawili wa huyo Prime Minister. Na tukasem Prime Minister ndiye atachagua Cabinet. Sasa mmeanza kusikia sio hivyo, sio hivyo. Lakini hayo yote ni sawa, kwa maana you must have something ambayo unaweza ku-criticize. Tusingalisema hivyo, msingalisema hivyo, mwingine asingepata nafasi ya ku-criticize na kusema la, hii ikiwa hivi na hii iliwa vile, sasa mambo yatakuwaje? Ndio maana yake tunakuwa na ile National Conference ili sehemu zingine ziangaliwe sawa sawa. Hapa kweli ikifanywa hivi, hapana, hapa hata ingawa tulitoa mawazo namna hivyo mimi nimeona kwamba mambo yangukuwa namna hivi.

Mlituambia kwamba wabunge wawe wabunge tu. Si mlituambia hivyo? Na kwamba Ministers wawe professionals kwa maana mmepata, tukawauliza ni kwa nini mnataka namna hivyo? Mkatuambia tunaopata Ministries being guided or led by unprofessional Ministers. Wengine hata hawajui inaelekea wapi, na kwa hivyo tumetaka professionals walead Ministries. Na sisi tukasema tutafanya hivyo, tumeandika hivyo kwamba Ministers watoke nje ya parliament na wawe professionals. Lakini sasa nimeanza kusikia, ninasikia jinsi mambo yanakuja. Na jinsi yanavyokuja, that is very healthy kwa maana lazima uwe na kitu ambacho mwingine atatoa makosa.

Mlituambia tukatishe Ministries, mkate mpaka fifteen, tumekata. Ninadhani leo asubuhi nimesikia pahali fulani, sijui ni katika redio au nimesoma kwa newspaper, mwingine akisema zingekuwa ishirini. Unaona? Hayo ni mambo ambayo ni healthy, wacha watu waongee. This is what the debate is all about for people to look into the matters ndipo watuambie jinsi mambo yalivyo.

Na tena mkatuambia kwamba mumetaka two Houses of parliament, mumetaka Upper House na Lower House na tumeweka. Kutakuwa na Lower House na Upper House. Na kwa hivyo mtaweza kuangalia haya mambo na muanze ku-form opinion. Hii kweli, hii kweli uchumi wetu utabeba hii? Uchumi wetu utabeba hii? Hayo mambo yote tumeweka.

Tumeweka pia mambo juu ya mahakama. Mlituambia mahakama yanawasumbua, mahakama yamekuwa corrupt. Na saa hii

ninapozungumza, leo ni siku yetu ya kuwa kortini na mimi niko hapa Ekerenyo. Sijui kama nitabebwa juu kwa juu toka hapa au namna gani tuko kwa contempt. Lakini leo ni siku yetu ya kupelekwa kortini kwamba tulisema majaji wanafanya mambo mabaya. Kwa hivyo tuliposema mambo mabaya yanapatikana katika ma-court tumeshtakiwa, tumekosea. Lakini sio sisi, ni nyinyi mliotambia, ni nyinyi mlisema. lakini unajua mtu ambaye anatoa maneno katika mdomo au aliyefanya maandishi ndiye anashikwa sio wale waliomwambia. Lakini tunajua Wakenya wote walitambia na haya ni mambo ambayo yako dhahiri.

Tumesema mtu akishikwa afikishwe kortini na kesi yake ifanywe na competent, qualified people. Watu wasiwe wanapelekwa pelekwa tu mambo yanaishia kwingine na yameishia kwingine. Promotions zifanywe na njia inayofaa na pia iwe through professionalism. Na watoto kama hawa pia tulisema walindwe hapa without discrimination. Huyo ndiye Mkenya wa kesho, wa leo na kesho. Kwa hivyo tukasema hao watoto walindwe kabisa, kabisa. Watu wasiwafanyishe watoto kazi. Tunaposema kazi, ni ile kazi ngumu ambayo mtoto asingeweza lakini kwa maana anasumbuka analazimika kuifanya. Hakuna ubaya wa kazi, kazi kuna dignity of labour na kuna kazi ambayo ni ya kuumiza ambayo haikufaa. Mtoto kufanyishwa kazi asiende shule kwa mfano.

Tukasema watoto ni lazima wasomehswe, mliutambia hivyo. Na mkasema watoto wapate elimu ya bure and compulsory kwa primary schools. Mkatuambia waalimu wa nursery walipwe kwa maana hao ndio waanzilishi wa elimu. Kwa hivyo mambo yenu yote mtakaposoma katika hiyo draft, mtayapata. Na kuna vijitabu vingine, hebu ni muulize Co-ordinator. Unavingapi hivi/

James Masaki Mong'are: Bwana Commissioner we have twenty of these (?).

Com. Ayonga: Na how do you make them accessible?

James Masaki Mong'are: Because of that limited number we thought that we shall first limit them to the documentation centre. The twenty of them are not even enough for the CC members.

Com.Pastor Ayonga: Okay, lakini hizo twenty zitagawa namna gani? Kuna documentation center hapa?

James Masaki Mong'are: In Nyamira.

Com.Pastor Ayonga: Hiyo tu?

James Masaki Mong'are: Yeah.

Com. Ayonga: Sasa hawa watu wa Ekerenye wawe wanaedna mpaka Nyamira kusoma?

James Masaki Mong'are: Well, that is the arrangement we have had all through, maybe we will think of something else when we have enough books.

Com. Ayonga: Kwa maana, let me suggest this, we are going very first and there is no time to waste. Kama una twenty, si kumi zingebaki hapa na zingine ziende Nyamira?

James Masaki Mong'are: But how shall we share the ten?

Com. Ayonga: Sasa hiyo ni internal administration. Hiyo sasa mtagadiliana kati yenu, si kuna watu wa 3C's hapa?

James Masaki Mong'are: Who are more than ten...

Com. Ayonga: Sindio, wako hapa? Si mnaweza kufanya your internal administration hapa na kukubaliana pahali hivyo vinaweza kuwekwa. Sio ati mtu abebe aende nacho Nyumbani kwake lakini pahali ambako mtu akifika atasoma na aende ID aache kitabu hapo.

Ninadhania kwamba ofisi yetu inaedelea kuchapisha vingine. Nikwambie we are going very fast na hata machine zinawaka moto. Ukifikiria tuna constituency mia mbili na kumi, halafu kuna institutions, halafu kuna nini, na ndipo ufikiri kila moja ipate ni work na ni money. Na tunajua tunakimbizwa na tunataka kukimbizana na wanaotukimbiza. Kwa hivyo the few you get kama mnaweza kushare, kwa mfano leo hivi kila mmoja wenu, nikuja nikasema kila mmoja wenu halafu zitakosekana.

Lakini I think those who have come and who have registered watapata a copy ya Draft Constitution ya kuweza kuenda nayo. Kwa hivyo ukipata, uende uisome. Na yule mzee mwignine anakaa kando yako, mwite kuja tusome Katiba iko hapa, njoo tusome. Njoo tujadiliane. Na wakati ambao mnakutana wherever you are, ongea juu ya hiyo, ambayo mmeona kwamba haikufaa, jadiliana juu ya hiyo ambayo unaona haikukazwa. So that in this one month ambayo tayari karibu wiki moja inakwenda, iwe kwamba we are informed about what we had given views for.

Halafu mlituambia juu ya independence of the judiciary. Mkatuambia kwamba judiciary ya sasa jinsi ilivyo, independence yake imenyang'anywa na executive. Mkasema sometimes wanaingiliwa na mkasema mnataka judiciary ambayo ni independent. Na mkasema njia ya kuweza kuifanya independent ni kwamba the appointment of judges iwe vetted na parliament. Na sisi tukaenda tukaweka hivyo, tuka kaza nut hiyo na kusema yeyote ambaye anapandishwa cheo, magistrate anayekuwa judge lazima jina lake linaweza kuwa recommended lakini anayesema la mwisho ni nani? Ni Parliament. Parliament inaweza kukataa na kusema hapana leta jina lingine, this person is not qualified. Au mtu huyu sifa zake ziko hivi na hivi, huyu mtu hawezi kuwa a judge in the High Court.

Mkatuambia tena kitu kingine, mnataka Supreme Court, si mlituambia? Nasi tukaenda tukaitwanga tukaweka, Wakenya wamsema wanatka Supreme Court. Na hiyo iko hapo. Na tena tukaweka kwamba lazima kuwe na Judicial Commission ambayo inaangalia mambo ya judiciary. Ya watu ambao ni wasomi, watu ambao wanajua mambo ya makorti, mahakama, jinsi yanavyofanya kazi na ilindwe namna hivyo. Iweze kuwa independent ya any other arm of the government, na tukafanya hayo.

